# MAPITIO YA MWENENDO WA SOKO KWA WIKI 03 JANUARI 2025

**KARIBUNI TENA KATIKA KIPINDI CHETU CHA KILA WIKI KINACHOKUHABARISHA KUHUSU MWENENDO WA SOKO LA HISA LA DAR-ES-SALAAM, NA KULETWA KWENU NA VERTEX INTERNATIONAL SECURITIES, PAMOJA NANYI LEO NI MIMI, FRANCO ATILYO**

Kwa wiki inayoishia tarehe 10 January 2025, mauzo katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) yaliongezeka kwa asilimia 130.56 kutoka TZS 3.5 bilioni bilioni hadi TZS 8.2 bilioni. Kiasi cha hisa zilizouzwa kiliongezeka pia kutoka hisa milioni 3 hadi hisa milioni 8.8 sawa na asilimia 193.5.

Jumla ya Mtaji wa Soko uliongezeka kwa asilimia 0.82, kutoka TZS 17.95 trilioni hadi trilioni 18.1. Mtaji wa Soko la Ndani ulipungua kidogo kwa asilimia 0.07, hadi TZS 12.215 trilioni kutoka TZS 12.224 trilioni kutokana na kupungua kwa bei ya hisa za AFRIPRISE, CRDB, na SWISS.

CRDB imeongoza kwa mauzo ya hisa wiki hii ikirekodi TZS 5.26 bilioni, ambayo ni 64.22% ya mauzo yote ikifuatiwa na NMB kwa asilimia 34.23 ya mauzo yote.

Kuhusu bei, hisa za AFRIPRISE zilipungua kwa TZS 5 wakati za DSE ziliongezeka kwa TZS 5 huku CRDB ikishuhudia hisa zake zikipungua kwa TZS 10 wiki hii. Hisa za SWISSPORT nazo zilipungua kwa TZS 100 wakati hisa za DCB zilipanda kwa TZS 5.

Jumla ya hisa milioni 5.62 za CRDB na hisa laki tano za NMB ziliuzwa kupitia kaunta ya makubaliano ya kabla huku wawekezaji wa ndani wakiendelea kutawala mauzo ya soko ya wiki nzima. Tunatarajia kuongezeka kwa mwitikio utakaoakisi kwenye mauzo ya hisa na bei kwa wiki zijazo.

Katika wiki kulikuwa na miamala 38 kwenye soko la hatifungani, ambapo soko lilisajili takribani TZS 6.33 bilioni.

Mnada wa hatifungani ya Serikali ya miaka 25 yenye namba 666 uliofanywa na Benki Kuu ya Tanzania tarehe 8 Januari 2024, ulisajili zabuni 904 kwa kiasi cha TZS 489.5 billioni ambapo zabuni 757 zilifanikiwa na kukusanya kiasi cha TZS 348.8 bilioni.

**MPAKA HAPO TUMEFIKIA MWISHO WA MAPITIO YA SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM KWA WIKI ILIYOISHIA IJUMAA YA JANUARI 10, 2025. MPAKA WAKATI MWINGINE MIMI NI FRANCO ATILYO**